# *BARUA #05; MWONGOZO WA KUFANYA MAAMUZI SAHIHI.*

Habari rafiki yangu mpendwa,

Karibu kwenye barua yetu hii kwenye mfululizo wa barua za mwaka wa mafanikio 2020/2021.

Barua ya leo nakwenda kukushirikisha mwongozo sahihi kwako kutumia ili kufanya maamuzi ambayo ni bora kwa mafanikio yako. Utajifunza hapa hatua sahihi za kuchukua ili kufika kwenye maamuzi yenye tija kwa mafanikio yako.

Lakini kabla ya kuingie kwenye mwongozo wa kufanya maamuzi, nina jambo fupi la kukushirikisha.

Rafiki, kuanzia mwaka huu wa mafanikio 2020/2021 nimechagua kufanya kazi na watu

wachache ambao wamejitoa kweli ili kufikia mafanikio makubwa. Watu ambao wapo tayari kujifunza na kuchukua hatua ili kufika kwenye mafanikio makubwa.

Wale ambao hawajajitoa kweli kufanikiwa, sitaweza kwenda nao kwenye KISIMA CHA MAARIFA. Hivyo kwenye tathmini za kila mwezi unazonishirikisha, kuna mengi nitakuwa nakushauri kwenye hatua za kuchukua, hivyo nategemea uwe unachokua hatua za kukuwezesha kufanikiwa zaidi.

Siyo lazima ufanye kila ninachoshauri, lakini angalau uwe na hatua unayochukua ambayo inazalisha matokeo yanayoonekana.

Nimechagua kuwekeza zaidi kwako, kukuwezesha ufike kwenye mafanikio makubwa kwa sababu mafanikio yako ndiyo mafanikio yangu. Hivyo kama unataka tuendelee pamoja kwenye hii safari, jifunze, chukua hatua na nioneshe matokeo ambayo unayapata.

Baada ya kukumbusha hayo machache, sasa karibu kwenye barua yetu ya mafanikio.

# *KISIMA MENTAL MODEL; MWONGOZO WA KUFANYA MAAMUZI*

## UTANGULIZI.

Ufanyaji wa maamuzi sahihi katika wakati sahihi ni hitaji kubwa kwenye mafanikio.

Wale wanaofanikiwa sana kwenye maisha siyo wenye akili sana, wala wanaofanya kazi kwa juhudi zaidi, bali wale wanaofanya maamuzi bora na yenye manufaa kwenye hali wanayokuwa wanapitia.

Ukichukua mfano wa kampuni au taasisi kubwa, mkurugenzi mkuu (CEO) analipwa zaidi ya mara kumi ya mshahara anaolipwa mfanyakazi wa chini. Ukipima ufanyaji wa kazi za nguvu, mfanyakazi wa chini atakuwa anafanya kazi za nguvu zaidi kuliko CEO, lakini CEO analipwa zaidi kwa sababu yeye ndiye anayefanya maamuzi.

Kabla hujaweka juhudi kubwa kwenye jambo lolote lile, lazima kwanza uhakikishe ndiyo jambo sahihi kwako kuweka juhudi na ili kujua usahihi wa jambo lazima uweze kufanya maamuzi bora.

Kwa kutumia mfumo wa kufanya maamuzi wa KISIMA MENTAL MODEL, tunaweza kufanya maamuzi sahihi katika wakati sahihi na yakawa na manufaa kwenye hali tunayopitia kitu kitakachotuwezesha kufikia mafanikio makubwa.

## CHANGAMOTO KWENYE UFANYAJI MAAMUZI.

Kufanya maamuzi sahihi katika wakati sahihi imekuwa ni changamoto kubwa kwa wengi. Hiyo ni kwa sababu kuna mambo huwa yanaingilia kati wakati wa ufanyaji maamuzi na kumfanya mtu ashindwe kufanya maamuzi sahihi.

Kuna vikwazo mbalimbali ambavyo vinaathiri ufanyaji wa maamuzi, lakini vikubwa zaidi ni hivi vifuatavyo;

## HISIA.

Hisia zikiwa juu, uwezo wa kufikiri unashuka na hapo mtu hawezi kufanya maamuzi sahihi.

Hivyo ni muhimu kuweza kutuliza hisia zako wakati wa maamuzi au kuepuka kufanya maamuzi mpaka pale hisia zitakapotulia.

Hisia zozote zile, chanya (kama furaha iliyopitiliza) au hasi (kama hasira au huzuni) huwa zinaathiri ufanyaji wa maamuzi.

## UJINGA.

Kile usichojua huwa ni kikwazo kwenye kufanya maamuzi.

Ili uweze kufanya maamuzi sahihi unapaswa kuwa na maarifa ya msingi ya kile unachofanyia maamuzi.

Usijidanganye unajua, hakikisha unajua kweli, hasa yale ya msingi kwenye eneo hilo, hayo yatakusaidia katika kufikia maamuzi sahihi.

## UPOFU.

Ujinga ni kile usichojua na unajua hujui, upofu ni kile usichojua, ila hujui kwamba hujui.

Kila mtu kuna eneo ana upofu, kwa Kiingereza inaitwa Blind Spot, hili ni eneo ambalo hujui kama una udhaifu. Wewe kwako unaona ni sawa, ila wengine wanaona siyo sawa, na wako sahihi.

Kwa walio wengi huwa wanakataa kujua eneo hili ambalo wana udhaifu na hivyo kuathiri sana maamuzi wanayoyafanya.

Wewe jua upofu wako uko wapi, jua ni udhaifu upi umekuwa nao katika kufanya maamuzi na wakati wa kufanya maamuzi jikinge eneo hilo lisiwe na athari kwenye maamuzi.

## MAZOEA.

Mazoea kwenye kufanya maamuzi yamekuwa chanzo cha kufanya maamuzi mabovu. Kila hali huwa inatofautiana na hali nyingine, kila changamoto unayopitia ni tofauti kabisa na changamoto nyingine, hata kama kwa nje zinaonekana kufanana.

Ili kufanya maamuzi bora, achana kabisa na mazoea, iangalie hali kama ilivyo na futa chochote ulichozoea kufanya. Anza upya kama vile ndiyo mara ya kwanza kwako kupitia kitu hicho na hapo utaweza kufanya maamuzi sahihi.

## KUFUATA MKUMBO.

Kufanya maamuzi kwa kuiga yale ambayo wengi wanafanya na sababu nyingine inayopelekea wengi kufanya maamuzi mabovu. Huwa ni salama kufanya kile kinachofanywa na wengi kuliko kufanya kilicho sahihi. Ukikosea ndani ya kundi haiumizi kama ukikosea mwenyewe, ndiyo maana wengi hupenda kufuata mkumbo.

Siku zote jua kwamba kinachofanywa na wengi huwa siyo sahihi kwako kufanya, hivyo katika kufanya maamuzi, epuka sana kufuata mkumbo. Acha kabisa kuiga kile wengine wanafanya. Unaweza kujifunza kwa wengine wanafanyaje maamuzi yao, lakini usiige kile wanachofanya, fanya maamuzi yako kulingana na kile unachokabiliana nacho.

# MAKOSA YA KISAIKOLOJIA YA KUEPUKA KWENYE MAAMUZI.

Akili zetu wanadamu, huwa zinapendelea kujenga tabia ili kupunguza maamuzi ambayo mtu anafanya. Kitu kinapojirudia rudia, akili inakariri hatua za kuchukua na baadaye mtu unajikuta unachukua hatua kabla hata ya kufikiria.

Njia hii ya mkato ya kufanya maamuzi imekuwa inaathiri sana maamuzi ambayo tunayafanya. Hivyo ili kuepuka kufanya maamuzi yasiyo sahihi, lazima tuyajue makosa ya kisaikolojia yanayoathiri maamuzi tunayofanya.

Hapa kuna makosa 28 ya kisaikolojia ya kuwa makini nayo wakati wa kufanya maamuzi.

# MCHAKATO WA KUFANYA MAAMUZI.

Katika kufanya maamuzi, unapaswa kuwa na mchakato ambao unaufuata. Kwa kufuata mchakato huo unahakikisha vigezo mbalimbali vimezingatiwa ili kujiepusha kufanya maamuzi yasiyo sahihi.

Hapa kuna mchakato sahihi wa kufuata wakati wa kufanya maamuzi.

## ELEWA KWA UNDANI.

Kujua tatizo ni nusu ya kulitatua. Unaweza kushangaa lakini wengi wanaosema wamekwama kwenye kufanya maamuzi, hawajui hata ni tatizo gani wanalokabiliana nalo.

Hivyo hatua ya kwanza kabisa katika kufanya maamuzi ni kujua kwa undani tatizo au changamoto inayokukabili ambayo unapaswa kuifanyia maamuzi.

Jua kwa kuuona ukweli na siyo kuona kile unachotaka kuona.

## MATOKEO UNAYOTAKA.

Baada ya kulijua tatizo, kitu kingine muhimu unachopaswa kujua ni matokeo unayotaka kupata kwenye maamuzi unayokwenda kufanya.

Jua kwa hakika nini unachotaka kupata au kufikia. Pata picha kubwa ya matokeo

unayotarajia kuyapata ambayo yatakuwa na tija kwako.

Kwa kifupi hapa unaona kabisa nini unachotaka kupata au kufikia.

## FIKIRI KINYUME.

Baada ya kujua nini unachotaka kupata au kufikia, fikiria kinyume chake. Jua nini ambacho hutaki kupata au kufikia, yaani ni matokeo gani ambayo hutaki maamuzi yako yazalishe.

Ukishajua kile ambacho hutaki kupata, jua ni nini ukifanya utafika kwenye matokeo hayo na epuka kukifanya. Jua ni makosa gani unaweza kuzalisha na nini ukifanya kitazalisha makosa hayo kisha kiepuke.

Watu wengi wanapofanya maamuzi huwa wanaangalia tu matokeo wanayotaka kupata na kusahau upo uwezekano mkubwa wa kupata matokeo wasiyotaka kupata.

Hivyo katika mchakato wako wa kufanya maamuzi, jua ambapo ukienda utakufa na epuka kwenda hapo.

## KUWA KWENYE AFYA NJEMA.

Ili uweze kufanya maamuzi sahihi, lazima afya yako iwe njema. Na hapa inahusisha afya ya akili, mwili na roho.

Kwenye afya ya akili hakikisha ufikiri wako uko sahihi, akili na utashi havijachoka, huna kilevi chochote na pia hisia zako haziko juu.

Kwenye afya ya mwili hakikisha huna maumivu yoyote, huna uchovu, huna njaa kali na wala hujashiba sana.

Kwenye afya ya roho hakikisha una upendo kwako, kwa wengine na kwa kile unachofanya.

Katika mchakato wako wa kufanya maamuzi, zingatia sana haya ya kiafya, maana yasipokuwa sawa, itaathiri sana maamuzi yako.

## JIFUNZE KWA WENGINE.

Kwenye hali yoyote ile unayopitia na unataka kuifanyia maamuzi, jua kuna wengine ambao walishapitia hali kama hiyo na kuifanyia maamuzi. Wapo waliofanya maamuzi mazuri na

yakawasaidia na wapo waliofanya maamuzi mabovu na yakawaangusha.

Chagua watu ambao utajifunza kupitia wao kwa hali walizokuwa wanapitia na maamuzi waliyoyafanya. Kisha jifunze mambo ya kuzingatia katika kufanya maamuzi yako.

Muhimu sana ni usiige maamuzi, jifunze na siyo kuiga.

## KUWA NA CHUJIO.

Unahitaji kuwa na chujio la kurahisisha zoezi lako la kufanya maamuzi. Kwa sababu mambo yanayotaka uyafanyie maamuzi ni mengi na muda wako hautoshi kufanya mchakato huu kwa kila jambo, kuwa na kigezo ambacho unapimia hali au jambo linalohitaji kufanyia maamuzi.

Chujio hili linapaswa kutokana na wewe mwenyewe, kwa kujua nini kilicho muhimu kwako, maeneo gani unayoyawekea umakini zaidi na uimara wako uko wapi.

Ukishajua nini unataka kwenye maisha yako na kujua njia ya kufika kwenye kile unachotaka, chochote ambacho hakihusiki na hilo huna hata haja ya kupoteza muda wako kufanyia maamuzi, maana hakiendani na unachotaka.

## MISINGI YA KUZINGATIA WAKATI WA KUFANYA MAAMUZI.

Wakati unafanya maamuzi muhimu kwenye maisha yako, zingatia misingi hii iliyopo hapa. Kuna misingi ambayo inaingia kwenye kila aina ya maamuzi na kuna misingi inahusika kwenye baadhi ya maamuzi ila maamuzi mengine haipo.

Ni muhimu uijue misingi hii yote na kwa kila maamuzi unayofanya, kabla hujafikia hitimisho, pitia kila msingi kuona ni kwa namna gani umeuzingatia.

### UPENDO.

Kila unachofanya, ongozwa na upendo, maamuzi yanayotokana na upendo ni maamuzi bora kabisa.

Upendo ni kwako binafsi, kwa wengine na kwa kile unachofanya. Epuka kufanya maamuzi kama huna upendo ndani yako.

## UHURU.

Kila maamuzi unayoyafanya, yanapaswa kukuweka huru zaidi. Hivyo kabla hujafikia maamuzi jiulize je yanakupa uhuru zaidi au yanakubana zaidi.

Kama kuna njia mbili mbele yako, moja inakulipa kidogo lakini inakupa uhuru zaidi na nyingine inakulipa sana ila inakunyima uhuru, weka kipaumbele kwenye uhuru.

## FURAHA.

Furaha ni msingi muhimu wa kuzingatia katika kufanya maamuzi. Furaha ni matokeo ya vitu vingi, uhuru, amani na utulivu wa ndani vinahitajika sana ili uwe na furaha.

Maamuzi yoyote unayoyafanya, hakikisha yanakupa majuto kidogo au hayana majuto kabisa. Kama utafanya maamuzi ambayo baadaye utayajutia, yatakunyima furaha kwa muda mrefu.

Hivyo kwa kila maamuzi unayotaka kufanya, jiulize nini utajutia kufanya au kutokufanya na hilo likuongoze kufanya maamuzi sahihi.

## UKWELI.

Mara zote ujue na kusimama kwenye ukweli. Siyo rahisi kuufikia ukweli, hasa pale unapokuwa unataka sana kupata matokeo fulani.

Hivyo katika mchakato wa maamuzi, kazana kujua ukweli ni upi, jinsi ya kuufikia na kusimama kwenye ukweli huo.

## FEDHA.

Kwa maamuzi yoyote unayofanya, fikiria yanagusaje upande wa fedha.

Na kwenye fedha kuna mambo manne ya kuzingatia;

1. Kipato, maamuzi yoyote unayoyafanya yanapaswa kuchangia kuongeza kipato chako zaidi.

2. Matumizi, maamuzi unayofanya yanapaswa kupunguza matumizi yako, kuhakikisha matumizi yanakuwa chini ya kipato.

3. Akiba, maamuzi yoyote unayofanya yanapaswa kuchagia wewe kuweza kuweka akiba zaidi, uwe na akiba ya kuweza kuendesha maisha yako hata kama kutatokea dharura mbalimbali.

4. Uwekezaji, maamuzi unayofanya yachangie wewe kufanya uwekezaji unaokua thamani na kuzalisha faida hata kama hufanyi kazi moja kwa moja.

## RIBA MKUSANYIKO.

Matokeo makubwa huwa hayatokei haraka, bali yanahitaji muda wa kujitengeneza na kukua. Kila hatua unayochukua haipotei, bali inajikusanya na kuja kuleta matokeo makubwa baadaye.

Kwa maamuzi yoyote unayofanya, usiangalie leo wala kesho, bali angalia miaka mingi ijayo. Kwa kila hatua unayotaka kuchukua, hata kama

ni ndogo, jua athari zake zinaendelea kukua kadiri muda unavyokwenda.

Hivyo fanya maamuzi ya kuchukua hatua sahihi bila kuacha huku ukiupa muda nafasi ya kukuza matokeo yanayopatikana.

## SIFA.

Sifa yako ndiyo kila kitu kwako, jenga na kulinda sifa yako kila wakati kwa kuwa huo ndiyo mtaji wa kwanza na muhimu kwako.

Katika kufanya maamuzi, zingatia sana sifa yako. Usifanye maamuzi yoyote yatakayoharibu sifa yako, hata kama yana manufaa makubwa.

Kwenye sifa pia chagua mtu unayemkubali sana kisha jipime kupitia yeye. Kwa kila hali ya kufanya maamuzi unayopitia, jiulize kama ingekuwa mtu huyo angefanya nini.

Kwa kuwa umejifunza kuhusu yeye na kumjua kwa undani, kujiuliza swali hilo kutakuonesha maamuzi bora kwako kufanya.

## MFUMO.

Kama kuna maamuzi unayoyafanya mara kwa mara, yatengenezee mfumo. Hii itarahisisha mchakato wa maamuzi yanayojirudia rudia.

Pia kwenye kila eneo la maisha yako, kuwa na mfumo unaoufuata katika kufanya maamuzi muhimu.

## GHARAMA.

Jua hakuna kitu cha bure, kila kitu kwenye maisha huwa kina gharama.

Katika kufanya maamuzi, jua gharama unayopaswa kulipa, kisha chagua kulipa gharama hiyo sasa.

Japo unaweza kuona fursa ya kukwepa gharama sasa, usifanye hivyo, lipa gharama sasa kwani ukija kulipa baadaye unalipa kwa riba.

Pia kama kuna njia au fursa mbili mbele yako, moja ni ngumu na nyingine ni rahisi, mara zote chukua iliyo ngumu. Maana kinachokuwa

kigumu mwanzoni, baadaye huwa rahisi, wakati kinachoanza kwa urahisi kuishia kuwa kigumu.

## JUMLA CHANYA.

Kwa kila maamuzi unayoyafanya, tengeneza jumla chanya (positive sum) na siyo jumla sifuri (zero sum). Jumla chanya ni pale unapofanya maamuzi yanayokunufaisha wewe na wengine pia (win-win) wakati jumla sifuri ni pale unapofanya maamuzi yanayokunufaisha wewe na kuwaumiza wengine (win-lose).

Kuna fursa nyingi za kila mtu kunufaika kwa maamuzi unayoyafanya, hivyo fanya maamuzi kwa kuzingatia kila anayehusika kunufaika. Kazana kutoa thamani zaidi kwa wengine kupitia maamuzi unayofanya.

## WATU WA KUSHIRIKIANA NAO.

Kuwa na kigezo cha kuchagua watu wa kushirikiana nao na kama mtu hajakidhi vigezo usijihusishe naye kwa sababu atakuumiza.

Kuna vitu vitatu muhimu vya kuangalia kwa kila unayetaka kujihusisha naye;

1. Akili, mtu anapaswa kuwa na uelewa kwenye kile anachokifanya na pia kupenda kukifanya.

2. Nguvu, mtu anapaswa kuwa kwenye afya njema ya kuweza kuchukua hatua anazopaswa kuchukua.

3. Uadilifu, mtu anapaswa kuwa na uadilifu wa hali ya juu, ambaye anafanya jambo sahihi wakati wote na kutimiza anachoahidi.

Zingatia vigezo hivi vitatu katika kuchuja na kuchagua watu wa kujihusisha nao.

## UDHIBITI.

Kuna mambo yako ndani ya uwezo wako na ambayo yako nje ya uwezo wako.

Katika kufanya maamuzi, jua yale yaliyo ndani ya uwezo wako na kuyafanyia kazi na yale yaliyo nje ya uwezo wako na kuachana nayo.

Haijalishi utahangaika kiasi gani, kama kitu kiko nje ya uwezo wako, hakuna namna unaweza kukiathiri.

Hivyo fanya maamuzi yako kwenye yale yaliyo ndani ya uwezo wako na yaliyo nje ya uwezo wako yapokee na ona jinsi unaweza kwenda nayo.

## NYENZO.

Kwenye kila maamuzi unayofanya, jua nyenzo (Leverage) ulizonazo na jinsi ya kuzitumia kufanya maamuzi bora.

Nyenzo ni kile kinachokuwezesha kutumia nguvu ndogo kuzalisha matokeo makubwa.

Nyenzo zinaweza kuwa watu unaowajua, rasilimali ulizonazo, fedha, uzoefu na ujuzi ulionao, teknolojia iliyopo na vingine unavyoweza kuwa navyo ambavyo vinazalisha matokeo makubwa.

## HATARI.

Kila maamuzi unayoyafanya huwa yana hatari ndani yake hivyo unapaswa kupima ukubwa wa hatari kabla ya kufanya maamuzi. Pia kwa kila maamuzi unayofanya, hakikisha unajua kiwango cha hatari, jinsi ya kupunguza hatari na pia kuepuka hatari isikupoteze kabisa.

Katika kufanya maamuzi kwa kuzingatia hatari simamia haya;

1. Uwezekano wa kupata uwe mkubwa kuliko wa kupoteza, angalau 90/10. Kama uwezekano wa kupata na wa kukosa unalingana, hiyo ni kamari, epuka sana kamari.

2. Unapopata, faida iwe kubwa kuliko hasara unayopata ukipoteza. Angalau faida iwe mara kumi zaidi ya kile ambacho unaweza kupoteza.

3. Usipoteze kila kitu, kwa hatari yoyote unayochukua, hata kama utapoteza basi hakikisha kupoteza huko hakukuangushi kabisa. Hivyo epuka hatari ambazo zinaweza kupoteza kila ulichonacho na kujikuta chini kabisa.

## SHERIA ZA ASILI.

Asili huwa inajiendesha kwa sheria zake ambazo huwa hazishindwi. Kwa sheria hizo asili huweza kukamilisha mambo yake yote bila ya haraka wala kuchelewa.

Kwa maamuzi unayotaka kufanya, angalia sheria zipi za asili zinahusiana na maamuzi

hayo. Pia angalia jinsi sheria za asili zinavyofanya kazi na jinsi unavyoweza kutumia mfano wake kufanya maamuzi sahihi.

Na muhimu kabisa, usifanye maamuzi yoyote yanayoenda kinyume na sheria za asili. Asili huwa haibembelezi, huwa inafuata sheria zake bila kuangalia nani anayedhurika. Kama umepanda juu ya ghorofa na kujirusha, utaanguka chini, hiyo ni sheria ya asili, haijalishi utakuwa unaogopa kiasi gani, asili inafuata sheria yake, haikuangalii wewe.

Kwa kuzifuata sheria za asili na kufanya maamuzi yako kwa kuiga mfano wa asili, utaweza kufanya maamuzi bora na sahihi.

## HITIMISHO.

Tumia mfumo huu wakati wa kufanya maamuzi, ili uweze kufanya maamuzi bora na sahihi kwa kile ambacho unapitia.

Tutaendelea kuuboresha mfumo huu wa maamuzi kadiri tunavyokwenda, hivyo karibu ushirikishe matokeo unayoyapata kwa kutumia

mfumo huu ili tuweze kuufanya kuwa bora zaidi, maana huu ni mfumo tutakaokwenda nao kwenye maisha yetu ya mafanikio.

## MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021